



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA



Tarehe: 21/02/2025


## TANGAZO

Mkurugenzi wa Jiji anawatangazia waombaji wote walioshiriki zabuni ya upangishaji wa maeneo ya biashara katika eneo la soko kuu mjini kati kuwa majibu ya awali yametolewa ambapo;

1. Wote walioandikiwa [**APEWE**] ndio wanaokusudiwa kupewa (Hii inawahusu wenye **ILANI** halali tu)
2. Wote walioandikiwa [**AINGIZWE KWENYE TAUSI AUCTION**] ni waombaji wapya (wasio na Ilani) waliokidhi vigezo vyote na wanaokusudiwa kushindanishwa kupitia mnada katika mfumo wa TAUSI. Vilevile mnataarifiwa kufika katika ofisi za Halmashauri ya Jiji kwa ajili ya kuendelea na taratibu za kusajiliwa katika mfumo wa TAUSI; Wahusika waje na vielelezo vifuatavyo;-
  - Namba ya **NIDA**,
  - Namba ya Mlipa Kodi (**TIN**),
  - **Namba ya Simu** iliyosajiliwa na NIDA ya mhusika na;
  - Taarifa Binafsi
3. Waombaji wote walioambatanisha Ilani halali zenye majina ya watu wengine wanaruhusiwa kuwasilisha malalamiko yao katika **DAWATI LA MALALAMIKO** lililo andaliwa na Halmashauri ya Jiji la Mwanza wakiwa na vielelezo vyao vyenye uthibitisho kuhusu Ilani hizo ndani ya muda wa kusudio uliotolewa katika zabuni hii.
4. Waombaji wenye ilani halali ambao maeneo waliyoomba yamegongana watahindanishwa kupitia mnada katika mfumo wa TAUSI. Hivyo waombaji waote ambao ilani zao zimegongana wanataarifiwa kufika katika ofisi za Halmashauri ya Jiji kwa ajili ya kuendelea na taratibu za kusajiliwa katika mfumo wa TAUSI; wakiwa na vielelezo vifuatavyo;-
  - Namba ya **NIDA**,
  - Namba ya Mlipa Kodi (**TIN**),
  - **Namba ya Simu** iliyosajiliwa na NIDA ya mhusika na;
  - Taarifa Binafsi

**N.B:** Kwa wale wote watakaoshindanishwa katika mfumo wa TAUSI kwa njia ya mnada hawatalipa **ADA YA ZABUNI** kwa hatua hii.

*Tangazo hili linahusu wale tu walioshiriki uombaji wa Zabuni ya upangishaji wa maeneo ya biashara katika eneo la Soko kuu.*

  
Peter Juma Lehhet  
KAIMU MKURUGENZI WA JIJI  
MWANZA

**MKURUGENZI WA JIJI LA MWANZA**